GRADI 5 -YEAR 2022
EXAMINATION: KISWAHILI

SEHEMU 1: KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA
Mwalimu amsomee mwanafunzi kifungu hiki kisha amwulize maswali yafuatayo.
Paka yuko jikoni. Amebeba panya mdomoni. Panya huyo ni mweusi. Paka anajificha mvunguni mwa meza. Mama anamwona paka.

i. Paka yuko wapi?
(Mwanafunzi ajibu)
ii. Paka amebeba nini mdomoni?
(Mwanafunzi ajibu)
iii. Panya huyo ni wa rangi gani?
(Mwanafunzi ajibu)
iv. Paka anajificha wapi?
(Mwanafunzi ajibu)
v. Nani anamwona paka?
(Mwanafunzi ajibu)

SEHEMU 2: KUSOMA KWA SAUTI (Alama 5)
Mwanafunzi asome kifungu hiki kwa sauti.
Ilikuwa siku ya Ijumaa tulipokuwa sebuleni tukitazama runinga. Sabu alianza kutusimulia jinsi ambavyo mwalimu wao alikuwa akiwaeleza kuhusu umuhimu wa miti. Hata ingawa alikuwa shuleni miaka sitini iliyopita, alikuwa akiyakumbuka vizuri.
Alianza kwa kusema kuwa mwalimu wao alisema kuwa miti huwa ni maskani ya wanyama mbalimbali sanasana nyuni ambao hutengeneza viota vyao na kutagia mayai humo. Aliendelea kutuambia kuwa wanyama wengine wanaotegemea miti kama makazi ni wanyamapori kama vile simba, chui, pundamilia na wengine.

SEHEMU 3: UFAHAMU (Alama 5).
Mwanafunzi asome kifungu hiki na kujibu maswali.

a. NDOTO YA AMINA
Babu alimnunulia Amina godoro na foronya. Usiku alipolala aliota ndoto. Aliota kuwa alikuwa msichana mkubwa. Alikuwa akifanya kazi ya ualimu. Baada ya miaka miwili aliacha ualimu akawa mkulima. Aliuza mazao akapata shilingi laki tatu. Alipokuwa akipeleka pesa zake benkini, aliamka kutoka usingizini.
i. Nani alimnunulia Amina godoro?
ii. Aliota ndoto wakati gani?
iii. Mara ya kwanza alikuwa akifanya kazi gani?
iv. Baada ya miaka miwili alianza kufanya kazi gani?